AJIRA, USTAWI NA
UJASIRIAMALI

MAELEZO SAHIHI

TAFSIRI ZA KUSAIDIA KUELEWA

- **Kizazi cha mapato:** Shughuli ambazo mtu hufanya ili kupata pesa. Uwezo wa kuzalisha mapato mara nyingi hutegemea ujuzi wako, rasilimali na mahusiano, na uwezo wako wa kuweka haya mambo yote pamoja ili kulinda ustawi wako. (Youth Livelihoods)
- **Ustawi:** ujuzi, rasilimali, uwezo na shughuli ambazo wewe na familia yako hujitahidi kufanya ili kuwa na kipato, kusaidia familia na kujenga thamani binafsi, kifamilia na kijamii. Ustawi unadhaniwa kuwa wa kufana ikiwa unaweza kuponea kutokana na mshtuko na mkazo, kwa mfano mavuno kupungua au mtoaji kuugua. (FAO)
- **Michanganyiko ya ustawi:** Mbinu au mkakati wa kuendeleza maisha yako kwa kuchanganya shughuli mbalimbali zinazozalisha kipato, ikiwa ni pamoja na kilimo, ujasiriamali, vibarua na shughuli za kijamii. Mkakati huu ni wa maana kama fursa za kazi ni za muda mfupi tu, kwa sababu inakuwezesha kuchanganya shughuli mbalimbali za kuzalisha mapato ili kuendelea kujikimu fursa zinapobadilika. (Invisible Lives)
- **Kaya:** 'Kikundi cha watu wanaokula kwenye chungu kimoja na kushirikiana pamoja ili kuboresha maisha na mali yao ya kifamilia kutoka kizazi hadi kizazi kingine. (FAO)
- **Ujasiriamali:** Kitendo cha kujenga biashara, kwa kutumia maarifa yako kutatua matatizo, hasa katika kutoa aina mpya ya bidhaa na huduma kwenye soko. Ujasiriamali hutokana na kuona njia mpya za kufanya mambo, au kuona nafasi ambayo watu wengine hawajaitambua. Unaweza ukawa mjasiriamali kwa sababu unahitaji kujitafutia ustawi. (Invisible Lives)
- **Ajira:** Katika sekta rasmi, ajira inamaanisha kuwa na kazi iliyo na baadhi ya manufaa ya ziada na ulinzi wa kiajira. Aina nyingine za ajira ziko katika sekta isiyo rasmi, ikiwa ni pamoja na kazi za vibarua na kazi za kilimo. Kwa mfano, kijana wa kike anaweza kupata pesa akifanya kazi kama fundi wa nguo akiwa nyumbani, akiwalea watoto wake na pia kufanya kazi katika shamba la familia yake wakati wa mavuno. Au anaweza kuwa na kibanda chake cha mboga sokoni, wakati pia anasaidia kuuza katika duka la jirani.
- **Kazi:** Shughuli zote unazofanya kwa ajili ya ustawi wako. Mfano wa kazi ni:
  - kibarua, kwa mfano kufanya kazi katika duka kwa kiwango fulani, ikihesabika kwa kila saa, siku, wiki au mwezi;
  - kazi ya kujitegemea, kama vile kuwa na kibanda chako cha chakula kwenye soko;
  - kazi ya kibarua, kwa mfano kufanya kazi shambani wakati wa mavuno;
  - kitengo au kipande cha kazi, kwa mfano kupewa kazi na mteja ya kumtengenezea viti 20 vya mbao.
- **Kujikimu:** Njia au mkakati wa kupata chakula na rasilimali kusaidia kuishi na ustawi. Kwa mfano, katika kaya nyingi nchini Tanzania zinazotegemea ukulima mdogo, familia hulima katika mashamba madogo ambayo yanaweza kukimu mahitaji yao ya chakula na lishe wakati njia za mapato ya pesa hukoma. Hata hivyo, kaya hizi zinaathirika zaidi na umasikini kuliko kaya zilizo na vyanzo tofauti tofauti vya mapato, kwa sababu zina nafasi chache tu za kukusanya pesa, kushirikishwa kifedha na kujijengea mali. Kaya zinazotegemea kilimo kidogo cha kujikimu huwa na uwezekano mkubwa zaidi wa kujikuta katika hali ya umasikini na kukumbwa na uhaba wa chakula ikiwa mavuno yao yataathiriwa na wadudu au ukame, na hawana pesa au mali inayoweza kuwakimu.

JE, WAJUA?

TANZANIA INA MASHAMBA MILIONI 3.7 YA HEKTA 2.2 ZA ARDHI AU CHINI. WATU MILIONI 19 WANAISHI NA KULIMA KATIKA MASHAMBA HAYA MADOGO

(FAO)

WENGI WA VIJANA WALIOHOJIWA KWA UTAFITI KUHUSU USTAWI NCHINI GHANA NA UGANDA WALIRIPOTI KWAMBA WAO WANGEPENDA KUWA NA BIASHARA ZAO WENYEWE KULIKO KUWA KWENYE AJIRA RASMI

(Invisible Lives)

Vijana nchini Tanzania ni 60% ya wafanyakazi, lakini pia wao hukosa ajira kwa mara mbili ya kiwango cha watu wazima, iwapo ni kutokana na ukosefu wa elimu na ujuzi

KUWA NA UJUZI UNAOFAA NI MUHIMU KWA KUFANIKISHA MKAKATI WA USTAWI. UTAFITI ULIOHUSISHA WAAJIRI ULIGUNDUA KWAMBA MAPATO YA VIJANA WENYE UJUZI YALIKUWA KARIBU MARA NNE ZAIDI KULIKO MAPATO YA VIJANA AMBAO HAWAKUWA NA UJUZI

(YouthMap 2014)

ASILIMIA SITINI YA WATU WASIOAJIRIWA NCHINI TANZANIA NI VIJANA

(YouthMap 2014)

KATIKA UTAFITI ULIOHUSISHA VIJANA WA TANZANIA AMBAO WALIKUWA WAKIFANYA KAZI, NI 4% TU WALIJIBU KWAMBA MAPATO YAO YALIKUWA YANATOSHA KULIPIA GHARAMA ZAO (YouthMap 2014)

Ni 3% tu ya idadi ya watu wanaofanya kazi nchini Tanzania wanaotambulika kama wenye ujuzi wa juu, na 84% ya idadi ya watu kutambulika kama wenye ujuzi mdogo tu (YouthMap 2014)

ASILIMIA 90 YA VIJANA WALIOHOJIWA KATIKA UCHUNGUZI WA HIVI KARIBUNI WALISEMA KWAMBA WALIKUWA NA SIMU ZA MKONONI

(YouthMap 2014)

MFUMO WA USTAWI WA KUDUMU

- Mfumo wa Ustawi wa Kudumu unaangazia njia nne muhimu za kuelewa jinsi watu wanavyoendeleza ustawi wao na kuweza kujiendeleza hali ya maisha yao ikiendelea kubadilika:
  - Mali watu wanayoitegemea, ikiwa ni pamoja na rasilimali za kijamii na vifaa, mtandao wa familia na marafiki; au mali ya mtu, mashine na ardhi;
  - Mikakati yao ya kudumisha ustawi inategemea mali yao; lakini pia muktadha wa kiuchumi, kwa mfano, ikiwa wameshirikishwa kifedha. Nchini Tanzania, wengi wa wakulima wadogo walio kwenye hali ngumu zaidi hawafikiwi hata na huduma za kifedha zile za msingi au zisizo rasmi, hivyo basi mara nyingi wanajikuta katika mapambano ya kila siku ya kujikimu maishani (J. Anderson, C. Marita & D Musiime; Mei 2016).
  - Muktadha ambao watu huendeleza ustawi wao hupindwa na sababu za kijamii, kiuchumi na kisiasa. Kwa vijana wengi nchini Tanzania hali ya kiuchumi ya ajira chache inaweza kufanya mkakati ule wa kuchanganya njia za ustawi kuwa mzuri ili kukabiliana na upungufu na kutokuwa na uhakika (UNISDR Livelihoods; Invisible Lives).
  - Mambo ambayo yanaweza kuimarisha au kudhoofisha ustawi wakati wa mshtuko au mkazo, kama vile ukame au mmomonyoko wa udongo unaoendelea kwa muda, mabadiliko katika uchumi, au kifo cha mtu aliyetegemewa (DFID, UNISDR Livelihood; FAO).
  - Kwa mfano, katika kaya nyingi Tanzania mshirika wa familia iwapo atakuwa mgonjwa, akiba ya pesa humalizika, na kuacha hiyo familia katika hatari zaidi ya kuwa maskini (Intermedia).

KUPATA PICHA (UELEWA) KAMILI YA USTAWI MCHANGANYIKO

- Kutokana na ukosefu wa ajira rasmi, vijana wengi Watanzania huchanganya shughuli tofauti kwa ustawi wao. Mkakati huu wa kujikimu huitwa ustawi mchanganyiko, na husaidia vijana kuingia na kutoka kwenye vibarua vya muda mfupi fursa zinapotokea. Kuendeleza ustawi wa njia ya mchanganyiko husaidia kupunguza hatari ya ukosefu wa ajira: ikiwa chanzo kimoja cha kazi kitasimama, basi itakuwa kuna vingine unavyoweza kuvitegemea. Na iwapo fursa mpya ya kazi nzuri itatokea, unaweza kuipata fursa hiyo bila kudhabihu (athiri) vyanzo vyako vingine vya ustawi, kwa mfano kwa njia ya kupunguza muda unaotumikia biashara yako, au kupata mtu wa familia kukusimamia majukumu yako.
- Mfumo wa ustawi mchanganyiko una sehemu nne: kilimo, ujasiriamali, kazi ya mshahara na mitandao ya kijamii:
  - **Kilimo** bado ndicho chanzo kikubwa cha ajira kusini mwa Jangwa la Sahara Afrika, ingawa mishahara huwa midogo. Licha ya baadhi ya mitazamo hasi kati ya vijana, kilimo kinabaki kuwa zalisho muhimu katika ustawi mchanganyiko, hasa kwa sababu kinatoa njia ya kujikimu wakati aina nyingine za kuzalisha mapato hufifia (Invisible Lives)
  - **Ujasiriamali** ni shughuli nyingine ambayo inaweza kuanzishwa kwa urahisi katika sekta isiyo rasmi, na inaruhusu kubadilika. Kwa mfano, mjasiriamali anaweza kupunguza nishati na rasilimali anazotoa kwa biashara yake wakati anahitajika kwengine zaidi, na kisha kuongeza juhudi zake tena wakati hahitajiki sana (Invisible Lives)
  - **Kazi** za mshahara mara nyingi huwa chache na za muda mfupi tu, lakini ni za muhimu sana kwa maisha ya vijana ambao wanaweza kuzipata (Invisible Lives)
  - **Mahusiano** ya kijumuiya ni mitandao ya wajibu, msaada na kubadilishana ambayo vijana hushiriki, na ni ya muhimu kuchangia jinsi wanavyopata fursa za ajira na ustawi. Kwa kushiriki katika maisha ya kiraia au siasa za mitaa, kwa mfano, vijana wanaweza kuunda mahusiano ambayo yataweza kuvutia fursa mpya za biashara au ajira. (Invisible Lives)

USTAWI MCHANGANYIKO, USTAWI ENDELEVU: UCHUNGUZI KIFANI

Hebu fikiria huu uchunguzi kifani wa hawa dada wawili wanaofuata njia ya ustawi mchanganyiko, kwa kutumia Mfumo wa Ustawi Endelevu kuangalia mali tofauti-tofauti, mikakati, muktadha na aina za ulinzi kutokana na mazingira magumu yanayoweza kuathiri maisha yao:

Amina amekuwa akifanya kazi ya kibarua katika kiwanda cha mikate kwa siku kadhaaPia husaidia dada yake, Maria, kulea watoto wake. Kila mwaka wakati wa mavuno anahitajika kushiriki kazi za mavuno ya mtama wa familia. Kazi ya nyumbani ambayo Amina anasaidia inamruhusu dada yake kuendesha biashara ndogo lakini yenye faida ya kuuza nguo na mikoba ya mitumba. Kina dada hawa hawajaweza kupata mkopo wa benki kwa sababu hawana hati miliki ya ardhi hiyo ya familia. Hata hivyo, wanapanga kuwekeza mapato ya mauzo ya mitumba, pamoja na mapato ya Amina kutoka katika kiwanda cha mikate, ili kuboresha shamba la familia na kugeuza ukulima wa kujikimu kuwa wa kuzalisha faida zaidi kwa mazao ya alizeti. Baadhi ya wanafamilia wana shaka na masuala haya, wakiamini kuwa nafasi ya mwanamke iko katika ndoa, kulea watoto na kutunza nyumba. Hata hivyo, mume wa Maria anamuunga mkono. Aliona ufanisi wa biashara yake ya mitumba. Dada hawa wanataka kununua vifaa vya kutengenezea mafuta ya alizeti ili kuuza katika soko la ndani.

Katika mfano huu, mali ya ustawi inaweza kujumuisha uhusiano mwema wa dada hawa kwa kuungana pamoja; ardhi ambayo familia hulimia; biashara yao ya mitumba; na ujuzi wao wa kilimo

Mkakati wao wa ustawi unategemea dada hawa wawili kuungana ili kuishinda changamoto waliyoipata ya kutojumuishwa kifedha na kutopata msaada wa familia kuwasaidia kuwa ‘wajasiriamali wa kilimo’. Mkakati wao pia unategemea ujuzi wao wa biashara (maarifa) na uwezo wao wa kuendeleza na kutumia ujuzi (wa mahusiano na wateja, elimu ya kifedha na kupanga malengo yao), pamoja na ujuzi mahususi katika kilimo na usindikaji wa chakula, ili kuwa na mafanikio katika shughuli mbalimbali za ustawi (Invisible Lives 2017)

Muktadha wao wa utsawi unaweza kuwa kwamba dada hawa wawili wanaona fursa katika uchumi wa ndani ya kuendeleza biashara katika mlolongo wa thamani wa alizeti, lakini pia wanakabiliana na masuala ya kutengwa kifedha pamoja na kutokana na desturi za kimila kuhusu majukumu ya wanawake. Hata hivyo, wanaweza kujaribu kujikusanyia pesa zinazotosha kuwekeza katika biashara yao mpya.

Dada hawa wanaweza kujikuta katika hali ya hatari ya mazingira magumu kutokana na changamoto kama vile mfumuko wa bei za mbegu, mashine na pembejeo au kushuka ghafla kwa bei ya mafuta ya alizeti; au ustawi wao unaweza kuhatarishwa iwapo mmoja wao atakuwa mgonjwa. Ili kupunguza hatari zao, wanaweza kufikiria kuchanganya na kuzalisha mazao mengine kwenye shamba lao, au kuendeleza fursa nyingine za biashara katika mnyororo wa thamani. Hata wanaweza kuendeleza biashara iliopo ya mitumba, ili kulinda ustawi wao kutokana na hatari za kuwa wajasiriamali.

MASWALI YA KUTAFAKARI

Ni mahusiano gani, mali na mikakati ipi ambayo itakusidia kukimu ustawi wako?

Ustawi wako una hatari zipi?

Kuna njia za kujilinda dhidi ya hatari hizi?

MALI YA USTAWI: MISINGI 5

Mali hizi zinaunda fursa na upatikanaji wa ustawi.

Mali ya kibanadamu inajumuisha ujuzi, uelewa, afya, uwezo wa kufanya kazi (UNISDR Livelihood). Utafiti wa hivi karibuni kuhusu ustawi wa vijana unaonyesha umuhimu wa kuendeleza ujuzi 'laini' ambao hutafsiri kutoka kwenye mazingira ya kazi hadi kwingine, kama vile ujuzi wa kuhesabu, mahusiano na wateja, kupanga malengo na kufanya maamuzi (Youth at Work; STRYDE)

Mali ya kijamii inajumuisha mitandao, uanachama katika makundi na mahusiano ya uaminifu ambayo huleta ushirikiano na fursa (UNISDR Livelihood). Watu wengi wana mitandao ya kijamii ambayo ina majukumu na fursa muhimu ambazo zinachangia jinsi wanavyofikia ustawi wao (Invisible Lives 2017)

Mali asili (Natural resources) inajumuisha ardhi, maji, udongo, misitu, uvuvi na zaidi (UNISDR Livelihood). Kilimo kinategemea msingi wa mali asili. Ili kuendeleza kilimo, ni muhimu sana kutunza mali asili.

Miundo mbinu (Infrastructure) inajumuisha barabara, nguvu, mitandao ya simu, zana, vifaa, na kadhalika (UNISDR Livelihood). Miundombinu hii inaweza kuathiri ustawi wako. Kwa mfano, ikiwa unafanya biashara ya kusafirisha mahindi kutoka masoko ya vijijini hadi mjini, hali ya barabara itakuwa na athari kubwa kwa ustawi wako.

Mali ya kifedha inajumuisha akiba, mapato, mikopo, utoaji malipo na vikundi, kama vile vyama vya mzunguko, vyama vinginevyo na miduara ya kupeanda zawadi (UNISDR Livelihood, InterMedia). Uwezo wako wa kupata/kufikia fedha pia una athari mkubwa katika ustawi wako. Kwa mfano, unaweza kujishirikisha katika kikundi cha akiba, ambacho kinakuwezesha kuhifadhi pesa ili kuwekeza katika elimu yako.

KILIMO KINATOA NAFASI ZAIDI ZA AJIRA KWA VIJANA

Hapa kuna sababu zinazoelezea ni kwanini:

1. Vikwazo ni vichahe. Makampuni madogo-madogo ya kilimo yanaweza kuanzishwa kwa urahisi, ukitumia umiliki mdogo tu, na yanaweza kusimamishwa na kuanzishwa tena kadiri inavyohitajika (Invisible Lives 2017).

2. Kuna fursa za vijana kujiajiri katika hatua zote za mnyororo wa thamani, kwa mfano kufuga kuku, uzalishaji wa maziwa au hata katika kutengeneza makaa ukitumia taka za kilimo (ULearn, Young African Entrepreneurs 2017).

3. Miji inakua, kumaanisha kuna watu wengi zaidi sasa katika miji wanaohitaji kupata chakula, na hii imejenga fursa mpya za biashara za kilimo katika uzalishaji wa chakula, usafirishaji na usindikaji, kama vile usambazaji wa chakula kwenye shule na vyuo, au kutengeneza vipodozi vya kiasili (Youth Think Tank Report 2016, Young African Entrepreneurs 2017).

4. Teknolojia za Habari na Mawasiliano, na hasa kusambaa kwa upatikanaji wa simu za mkononi, imeleta fursa mpya za biashara za kilimo na njia mpya za watu kupata huduma za kifedha na habari, kama vile bei ya sasa ya bidhaa sokoni (Youth Think Tank Report 2016).

VIUNGO KATIKA MNYORORO WA THAMANI: KUENDELEZA FURSA

Kilimo sio shughuli ya kujikimu tu. Kuna fursa nyingi za biashara katika kilimo, na fursa nyingi za vijana kujiunga na kizazi kipya cha 'wajasiriamali wa kilimo', wakijiajiri wenyewe katika shughuli tofauti za mnyororo wa thamani, ikiwa ni pamoja na uzalishaji, kutengeneza / kusafisha / viwango, kusafirisha, usindikaji / ufungaji / kuongeza thamani, kutafuta masoko / ubadilishi na biashara za rejareja:

- Amina anataka kuanza biashara. Mtama unalimwa kwa wingi katika jumuiya yake, na anadhani anaweza kuanzisha biashara nzuri ya unga wa uji wa watoto.

- John anaunda mtandao unaotumia simu za mkononi ili kuwawezesha makundi ya wakulima kuunganisha akiba zao na kuwekeza katika kuzalisha biashara mpya kwenye mnyororo wa thamani wa mtama na kuunganisha mawazo ya biashara kama ya Amina na masoko makubwa, hasa katika mitaa na miji inayoongezeka.

- Baraka anafanya biashara ndogo ambayo ina utaalamu wa kukusanya na kusafirisha mazao, ikiwa ni pamoja na mtama, kati ya mtandao wa kikanda wa maghala ya jumuiya ambayo yanaweza kuhifadhi mazao katika mazingira masafi ili kuepuka hasara za baada ya mavuno, ili wakulima wapate bei nzuri ya mazao yao.

KUPATA FURSA KATIKA MNYORORO WA THAMANI: UJUZI, UELEWA, RASILIMALI, FURSA NA HATARI

- **Uzalishaji:** yaani kukuza. Ujuzi na uelewa vinahitajika : kilimo, kutunza ardhi, kusimamia udongo, kuvuna, kutafuta soko, kuhifadhi kumbukumbu. Rasilimali zinazohitajika: ardhi, maji. Hatari zilizopo: ugonjwa wa mazao, ukame.

- **Kukusanya/kusafisha/kupanga kulingana na ubora:** Ujuzi na uelewa: ujuzi wa biashara, ujuzi wa kiufundi wa viwango, kutunza usafi. Rasilimali zinazohitajika: vifaa vya ghala, usafiri. Hatari zilizopo: hasara za baada ya mavuno.

- **Usindikaji / ufungaji / kuongeza thamani:** **Ujuzi na uelewa:** maandalizi na usindikaji, kutunza usafi, ununuzi, ujuzi wa biashara, uuzaji, kutafuta soko, kuhifadhi kumbukumbu. Rasilimali zinazohitajika: vyombo vya kazi, vifaa vya ufungaji wa bidhaa, wafanyakazi. Hatari zilizopo: kuoza na kuharibika, changamoto za manunuzi.
- **Masoko/biashara:** Ujuzi na uelewa: ujuzi wa biashara, mahusiano ya wateja, uhifadhi wa kumbukumbu za biashara. Rasilimali zinazohitajika: pesa, mahusiano ya kijamii na mitandao. Hatari zilizopo: bei ya chini kwenye masoko, kupungua kwa bei, wauuzaji-wa-kati au wakala/madalali (broker) kuingilia biashara, kutotimizwa kwa makubalianao ya biashara na kuchelewesha malipo au kutolipia bidhaa.

(NYENZO YA RASILIMALI)

ENDELEZA UTAFITI WAKO!

- **http://www.fao.org/docrep/008/a0273e/a0273e04.htm**
- **http://www.unisdr.org/files/16771_16771guidancenoteonrecoveryliveliho.pdf**
- **http://www.mastercardfdn.org/anzisha-prize-young-entrepreneur/**
- **http://www.mastercardfdn.org/wp-content/uploads/2016/06/MCF12013-Youth-ThinkTank-Report-digital-final.pdf**
- **http://www.mastercardfdn.org/wp-content/uploads/2017/02/Report_YouthLivelihoods_Feb2017.pdf**